

DCF inapochunguza ripoti ya unyanyasaji au utelekezaji wa watoto, ni lazima tuamue ikiwa mtu mwenye akili timamu angeamini kwamba jambo hilo lilifanyika. Ikiwa jibu ni NDIYO, ripoti inathibitishwa na jina la mtu huyo linaongezwa kwenye Sajili ya Ulinzi wa Watoto.

## Je, ni nini hujumuishwa kwenye rekodi ya sajili?

1. Jina la mtu huyo
2. Angalau sifa nyingine ya kusaidia kumtambua (k.m., tarehe ya kuzaliwa)
3. Tarehe na asili ya matokeo
4. Kiwango cha ulinzi wa mtoto kinachohusiana na hatari yake ya kuwadhuru watoto baadaye - kwa rekodi zote zilizoongezwa mnamo au baada ya tarehe 1 Julai 2009

## Je, watu wanaweza kufikia sajili?

La. Lakini waajiri wa sasa au wanaotarajiwa wanaweza kuipata ikiwa:

- ▶ Mtu anayekaguliwa atatoa ruhusa yake NA
- ▶ Kazi anayoomba inahusisha watoto, vijana au watu wazima wasioweza kujitunza

## Je, itakuwaje nikithibitishwa?

Jina lako litaongezwa kwenye sajili – isipokuwa kama utapinga uthibitisho wa madai na kufanya yabadilishwe.

## Je, kuwekwa kwenye rekodi kunaweza kuniathiri vipi?

Kunaweza kuathiri uwezo wako wa:

- ▶ Kuasili mtoto
- ▶ Kuwa mtoa huduma za utunzaji wa watoto
- ▶ Kutoa huduma za malezi/utunzaji unaomwezesha mtunzaji mkuu kupumzika
- ▶ Kufanya kazi au kujitolea katika nafasi zinazohusisha watoto, vijana au watu wazima wasioweza kujitunza

Watu wengine wanaweza kuomba rekodi yako ikiwa inafaa. Hii ni pamoja na:

- ▶ Mashirika ya ulinzi wa watu wazima/watoto
- ▶ Bodi ya Huduma za Matibabu
- ▶ Mawakili wa Jimbo

## UKAGUZI WA UTHIBITISHO WA SHUTUMA

Ikiwa ulithibitishwa:

- ▶ **Kuanzia tarehe 1 Januari 1992 hadi tarehe 31 Agosti 2007:**

Unaweza kuomba ukaguzi ili kupinga - wakati wowote.

- ▶ **Mnamo/baada ya tarehe 1 Septemba 2007:**

Unaweza kuomba ukaguzi ili kupinga - ndani ya siku 14 baada ya tarehe tulipokutumia barua ya kukujulisha kwamba:

- ⇒ Tunakusudia kuongeza jina lako kwenye sajili
- ⇒ Una haki ya kuomba ukaguzi wa uthibitisho wa shutuma

## Nini kitatokea nikiomba ukaguzi?

1. Tutawasiliana nawe ili kuratibu mkutano na mkaguzi huru.
2. Utakaporatibiwa, tutakutumia barua ya kuthibitisha mkutano na nakala za hati za uchunguzi zilizorekebisha (kulingana na sheria).
3. Baada ya mkutano, mkaguzi anaweza:
  - ⇒ Kuunga mkono uthibitisho
  - ⇒ Kubatilisha uthibitisho
  - ⇒ Kuielekeza DCF ifanye uchunguzi mpya
4. Utatumiwa barua ya uamuzi.
5. Ikiwa mkaguzi ataunga mkono uthibitisho:
  - ⇒ Tutaongeza jina lako kwenye sajili (*au kuendelea kuliweka ikiwa tayari lipo*)
  - ⇒ Unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa Bodi ya Huduma za Kibinadamu

### Ikiwa hutaomba ukaguzi kwa wakati unaoruhusiwa:

- ▶ Jina lako litaongezwa kwenye sajili (*au litasalia ikiwa tayari lipo*)
- ▶ Uamuzi utakuwa wa mwisho na hutakuwa na haki zaidi ya kuomba ukaguzi wa uthibitisho wa shutuma

## UKAGUZI WA UFUTAJI

Unaweza kuomba ukaguzi ili jina lako lifutwe (*liondolewe*) kwenye sajili mara tu baada ya idadi fulani ya miaka. Kipindi cha muda ambacho unapaswa kusubiri kinategemea:

- ▶ Ni lini ulithibitishwa
- ▶ Kiwango cha ulinzi wa mtoto wako (*ikiwa kipo*)

Soma ukurasa wa 1 wa [fomu iliyoambatishwa](#) ili upate maelezo kuhusu ni lini unaweza kuomba ukaguzi wa ufutaji. HUWEZI kuomba ukaguzi ikiwa unahitajika kuwa kwenye sajili ya wahalifu wa kingono.

## Nini kitatokea nikiomba ukaguzi?

1. Utapata fursa ya kuwasilisha taarifa kwa mkaguzi. Atazingatia mambo kama vile:
  - ⇒ Asili na idadi ya mara za uthibitisho
  - ⇒ Kipindi cha muda ambacho kimepita
  - ⇒ Ikiwa kuna uwezekano wa kutokea tena
  - ⇒ Mambo ambayo umefanya ili kubadilika
  - ⇒ Marejeleo ya tabia yako
2. Utaarifiwa kuhusu uamuzi huo, ambao unafanywa na Kamishna wa DCF.
3. Ikiwa ombi lako litakataliwa, unaweza kukata rufaa kwa Bodi ya Huduma za Kibinadamu.

## OMBA UKAGUZI

1. Soma ukurasa wa 1 wa [fomu](#) iliyoambatishwa ili kupata maelezo zaidi ikiwa unaweza kuomba ukaguzi kwa wakati huu.
2. Ikiwa unaweza, jaza ukurasa wa 2 wa [fomu iliyoambatishwa](#).
3. Jibu maswali kikamilifu na kwa usahihi. *Hatuwezi kushughulikia ombi lako isipokuwa liwe limekamilika.*
4. Onyesha aina ya ukaguzi unaoomba.
5. Tuma barua kwa:  
**Department for Children and Families  
Commissioner's Registry Review Unit  
HC 1 North, 280 State Drive  
Waterbury, VT 05671-1080**

**Ikiwa una maswali au unahitaji usaidizi, piga simu kwa (802) 241-2321.**

### Una haki ya:

- ▶ Kupata huduma za ukalimani bila malipo ikiwa una ujuzi mdogo wa lugha ya Kiingereza
- ▶ Kupata marekebisho adilifu ikiwa una ulemavu



## Sajili ya Ulinzi wa Watoto ya Vermont



SHIRIKA LA HUDUMA ZA KIBINADAMU  
IDARA YA WATOTO NA FAMILIA